

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



OFISI YA MAKAMU WA RAIS
MUUNGANO NA MAZINGIRA



BARAZA LA TAIFA LA HIFADHI NA USIMAMIZI WA MAZINGIRA

MWALIKO WA KUSHIRIKI KIKAO CHA KUKUZA UELEWA WA KANUNI ZA MAZINGIRA ZA UDHIBITI NA USIMAMIZI WA TAKA HATARISHI KWA WADAU WA UKUSANYAJI, USAFIRISHAJI NA UHIFADHI WA CHUMA CHAKAVU NA TAKA ZA KIELEKTRONIKI KITAKACHOFANYIKA SIKU YA JUMAMOSI TAREHE 10 JULAI, 2021 KATIKA UKUMBI WA MILLENIUM TOWERS ULIOPO ENEO LA MAKUMBUSHO, DAR ES SALAAM

Ofisi ya Makamu wa Rais ikishirikiana na Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) imeandaa mkutano wa wadau wanao jihusisha na shughuli za **Ukusanyaji, Uhifadhi, Usafirishaji, Urejelezaji Uingizaji nchini na Usafirishaji nje ya nchi taka hatarishi**. Mkutano huo umeitishwa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira, Mhe. Selemani Saidi Jafo siku ya Jumamosi tarehe 10 Julai, 2021 saa 3 asubuhi katika ukumbi wa Millenium Towers uliopo eneo la Makumbusho, Dar es Salaam.

Lengo la kikao hicho ni kukuza uelewa wa Kanuni za Usimamizi wa Mazingira za Taka Hatarishi na Taka za Kielektroniki za mwaka 2021 na kujadili changamoto katika Utekelezaji na Usimamizi wa Kanuni hizo. Aidha, wadau watapata nafasi kuainisha na kujadiliana changamoto mbalimbali na kutoa maoni ya kuimarisha udhibiti na usimamizi wa taka hatarishi.

Hivyo, tunawaalika wadau wote kushiriki mkutano huu muhimu kwa kujisajili kupitia namba zifuatazo: 0756 410 484 au 0682 446 030. Mwisho wa usajili ni tarehe 09 Julai, 2021.

Mha. Dkt Samuel G. Mafwenga
Mkurugenzi Mkuu
Julai 6, 2021